



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA FEDHA
MAMLAKA YA UDHIBITI WA UNUNUZI WA UMMA



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. FA.75/192/01/A/10

01 June, 2026

Kwa Taasisi Nunuzi Zote.

Tanzania Bara

Yah: **WARAKA NA. 1 MWAKA 2025/2026 WA KUANZA KUTUMIKA KWA MODULI
YA BODI YA ZABUNI KATIKA MFUMO WA NeST**

Tafadhali rejea kichwa cha habari hapo juu pamoja na Kifungu cha 32 cha Sheria ya Ununuzi wa Umma Sura Na. 410 ya Mwaka 2023, kinachoelekeza uanzishwaji wa Bodi ya Zabuni kwa ajili ya kuidhinisha ununuzi wa bidhaa, huduma, kazi za ujenzi na uondoshaji mali. Aidha, Kifungu cha 73 cha Sheria hiyo, kinaelekeza kuwa shughuli zote za ununuzi, ugavi na uondoshaji mali zifanyike kupitia mfumo wa kielektroniki.

2. Kwa kuzingatia matakwa hayo ya kisheria, Mamlaka ya Udhubiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) inapenda kuzijulisha Taasisi Nunuzi zote kuwa imekamilisha ujenzi wa Moduli ya Bodi ya Zabuni katika Mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma, yaani NeST.
3. Hivyo basi, Taasisi Nunuzi zote zinaelekezwa kuunda na kusajili Bodi zao za Zabuni ndani ya mfumo wa NeST kabla au ifikapo tarehe **30 Juni, 2026**.
4. Aidha, Taasisi Nunuzi zote zinajulishwa kuwa kuanzia tarehe **1 Julai, 2026**, michakato yote ya ununuzi inayohitaji idhini ya Bodi ya Zabuni kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi wa Umma na Kanuni zake, idhini hizo zitatakiwa kutolewa kupitia vikao vya Bodi ya Zabuni vitakavyofanyika kupitia Mfumo wa NeST. Hivyo, taasisi nunuzi haitaweza kuendelea na mchakato wa ununuzi iwapo Bodi ya Zabuni husika haitakuwa imeanzishwa na kusajiliwa kwenye mfumo wa NeST. Kwa ufafanuzi au msaada unaweza kutuma barua pepe kupitia support@nest.go.tz au kupiga simu namba 0736 494 948.

5. Nawatakia utekelezaji mwema.


Dennis K. Simba
MKURUGENZI MKUU